



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU



Unapojuibu tafadhali taja:

Kumb Na. F.10/3/VOL.III/59

09/11/2023

TANGAZO LA ZABUNI
ZABUNI NA. LGA/NDC/088/C/2023/2024/03
ZABUNI YA UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI MTENDAJI
NANYUMBU

Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji ambayo inatarajiwa kujengwa katika Makao Makuu ya Wilaya eneo la Ngarije Kata ya Kilimanihewa. Halmashauri inakaribisha maombi ya kazi kwa wananchi wenyewe sifa na uwezo wa kufanya kazi za ujenzi wa majengo ya Serikali kwa kutumia mfumo wa *Force Account*.

Masharti kwa waombaji

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Awe na uwezo wa kusoma ramani na michoro ya majengo na kuitafasiri vizuri
3. Mwenye uwezo usiopungua miaka Miwili (2) kwa kazi alizozifanya zinazofanana na kazi ya ujenzi wa majengo ya Serikali
4. Awe na idadi ya mafundi waisopungua Kumi (10) wenyewe uzoefu wa kazi za ujenzi
5. Mwombaji awe mwadilifu na mwenye kuheshimu maelekezo ya Mwajiri.
6. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha kwa ajli ya malipo ya mafundi wake kabla ya kufanyiwa malipo na Mwajiri.
7. Mwombaji asiwe na kazi nyingine maeneo mengine ili kuweza kukamilisha mradi kwa wakati.
8. Mwombaji asiwe Mtumishi au Kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.
9. Mwombaji atakayeshinda zabuni atafunga mkataba na Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa kazi iyo na kutakuwa na makato yafuatayo; -
 - a) 5% ya malipo ya ufundi kama kodi ya zuio (*Withholding tax*)
 - b) 0.3 ushuru wa huduma (*Service Levy*)
 - c) 5% fedha ya matazamio (*Retention*) ambayo baada ya kipindi cha meizi 3 itarejeshwa kwa fundi.
10. Ombi la kazi liwe na jina na anuani sahihi ya Mwombaji. Aidha Mwombaji aonyeshe mahali anapokaa (*Postal and Physical address should legibly and clearly be indicated*).

AKURUGENZI MTENDAJI
G. I. D. 2023

11. Mwombaji atalipa ada ya **Tshs. 50,000/=** kama ada ya maombi ya kazi na haitarudishwa (*None Refundable*). Malipo hayo yalipwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
12. Mwombaji atakayeshindwa kutimiza au kukamilisha maekelezo na masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye ushindani.
13. Mwombaji anawenza kuona na kukagua michoro ya jengo na mahali jengo litakapojengwa na kupata taarifa zingine kutoka ofisi ya Mhandisi wa ujenzi wa Wilaya
14. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Zabuni ziwasilishwe kwa mkono au kwa njia ya Posta kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 246,

NANYUMBU-MTWARA

15. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa barua barua **Pepe (e-mail)** hazitapokelewa.
16. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 15/11/2023 saa nne (4) asubuhi, na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kupokea zabuni hizo mbele ya waombaji watakao amua kuhudhuria kwenye ukumbi wa mikutano jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.



IBRAHIM J. MWANAUTA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NANYUMBU

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 246
NANYUMBU